**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI JIJINI DODOMA, TAREHE 1 MEI, 2022**

*Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu;*

*Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wengine mliopo;*

*Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Kattanga, Katibu Mkuu Kiongozi;*

*Mheshimiwa Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Wakuu wa Mikoa wengine mliopo;*

*Ndugu Tumaini Nyamhokya, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);*

*Ndugu Wellington Chibebe, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Ofisi za Afrika Mashariki;*

*Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;*

*Waheshimiwa Wabunge mliopo;*

*Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi;*

*Ndugu Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo; Ndugu Henry Mkunda, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA);*

*Ndugu Pendo Berege, Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri;*

*Ndugu Jayne Nyimbo, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE);*

*Ndugu Suzan Ndomba, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania;*

*Viongozi wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi;*

*Viongozi wote wa Vyama vya Wafanyakazi mliopo;*

*Viongozi na Maafisa wa Serikali mliopo;*

*Wawakilishi wa Vyama vya Siasa mliopo;*

*Ndugu Viongozi wa Dini;*

*Ndugu Wafanyakazi wenzangu pamoja na Wananchi mliokusanyika hapa;*

*Wanahabari;*

*Vikundi vya Wanahabari,*

*Mabibi na Mabwana.*

**Mshikamanooo ………. Solidarity ………!**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Kazi iendelee na nini? Na mishahara ndio kilio chenu, si ndio??**

Nianze kwa kumshukuru Mola wetu Mtukufu ambaye, kwa Rehema zake, ameturuzuku uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya Maadhimisho haya ya Siku ya Wafanyakazi Duniani. Haya ni Maadhimisho yangu ya pili ambayo nashiriki kama Mgeni Rasmi, tena mara hii tunafanyia hapa Jijini Dodoma, Makao Makuu ya Nchi. Hivyo nitumie fursa hii kuushukuru Uongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini kwa heshima hii kubwa. Vile vile niwapongeze TUCTA na Ofisi ya Waziri Mkuu Wizara ya

Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu kwa Maandalizi mazuri ya Sherehe hizi.

Nimejulishwa kuwa mwaka huu Maadhimisho haya yanaratibiwa na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) chini ya Katibu Mkuu, Ndugu Rashid Mtima na Mwenyekiti, Ndugu Tumaini Nyamhokya, ambaye ndiye rais wa TUCTA. Lakini natambua pia mchango mkubwa wa Mwenyeji wetu, Mheshimiwa Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Sekretarieti yake, pamoja na wakazi wote wa Mkoa wa Dodoma. ***Kwa kweli leo katika uwanja wa Jamhuri mambo ni Moto. Hongereni sana***

Niwashukuru pia wote, wadhamini waliodhamini shughuli hii, lakini na wengine wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kufanya maadhimisho haya kufana kiasi hiki.

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Kama mnavyofahamu, Siku ya Wafanyakazi huazimishwa kila mwaka duniani kote ikiwa na lengo la kutambua na kuenzi

mchango wa wafanyakazi katika maendeleo ya mataifa. Hivyo, nami nitumie fursa hii kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa jitihada na kujitoa kwenu katika kulijenga Taifa letu.

Bila shaka, mtakubaliana nami kuwa maendeleo yote yaliyofikiwa tangu nchi yetu ipate uhuru yanatokana na mchango wa wafanyakazi. Na kwa namna ya pekee, niwashukuru sana wafanyakazi wote kwa kuiunga mkono Serikali yenu katika kuwatumikia Wananchi na kuleta Maendeleo nchini.

Ndugu zangu niungane na Chama cha Waajiri (ATE) lakini pia ILO, kwanza nawashukuru kwa risala zao au hotuba zao nzuri mlizozisoma. Lakini niungane nao katika kuwatia moyo wafanyakazi kwamba waendelee kuzalisha, waendelee kuleta tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Lakini niwahakikishie pia kwamba, maoni na maombi waliyoyaleta mbele yangu leo tutayafanyia kazi ipasavyo.

Kabla sijaendelea zaidi, nitumie fursa hii pia kutoa salamu za pole kwa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri kufuatia wafanyakazi na waajiri waliopoteza maisha tangu tuadhimishe Sherehe za Mei Mosi Mwaka jana 2021. ***(Mwenyezi Mungu apumzishe roho zao, pahali pema peponi. Amina!).***

Halikadhalika, nitoe pole kwa kuwa hatukuweza kuepuka athari zilizosababishwa na changamoto kubwa za kidunia, hususan janga la korona lakini na hivi karibuni vita vya wakubwa huko Ulaya. ***(Na Wahenga walisema ''Mafahari wawili wanapopigana, zinazoumia ni nyasi. Japo kwa vita hii tumeumia nyasi lakini na wakubwa nao wanaopigana wameumia)***.

Kwa hiyo kwenye hili sio nyasi peke yetu, na kwa kweli majanga haya mawili yamesababisha ugumu wa Maisha hasa kutokana na gharama za kupanda kwa gharama za mahitaji muhimu ya wanadamu.

Hata hivyo, pamoja na changamoto kadhaa tulizopitia, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja nilichokabidhiwa usukani wa nchi yetu, tumeweza kupata mafanikio makubwa. Mathalan, tumetumia Shilingi **Trilioni 1.49** kutekeleza miradi mbalimbali katika sekta ya elimu, Shilingi **Bilioni 234.41** kwa ajili ya miundombinu ya afya, Shilingi **Bilioni 597** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara na Shilingi **Trilioni 1.4** kwa ajili ya maji mijini na vijijini. Muhimu zaidi, tumeendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi yote mikubwa, ikiwemo Ujenzi wa Reli lakini pamoja na Bwawa la Nyerere, pamoja na Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; tumetenga pia fedha ununuzi wa ndege **tano (05)**,

ikiwemo moja ya mizigo; ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege, na mengine mengi.

***Ndugu zangu:***

Hapa nimejaribu kutaja machache kati ya mafanikio mengi kutokana na ufinyu wa muda. Sijagusa sekta ya utalii, madini, ardhi, kilimo, viwanda, diplomasia, Utawala Bora, nk. Lakini nataka mtambue kuwa mafanikio haya yote na mengine ni matunda ya jitihada zenu na Serikali yenu. Na katika hili, ninazipokea kwa moyo shukrani pongezi mlizozitoa kwa Serikali yenu kwa ajili ya utekelezaji wa mambo mbali mbali ya maendeleo ya nchi. Pongezi zenu zinatupa moyo na hamasa mimi na wasaidizi wangu, kuendelea kufanya kazi kwa juhudi na kujitoa zaidi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Mbali na kutambua na kuenzi mchango wa wafanyakazi katika maendeleo ya Taifa, Siku hii hutumika kama Jukwaa la utetezi wa haki na maslahi ya wafanyakazi. Vile vile, kukumbushana juu ya wajibu wa Wafanyakazi katika kukuza Tija ndani ya nchi. Na hapa, nimesikiliza kwa makini risala iliyosomwa na **Ndugu Henry Mkunda**, Katibu Mkuu wa TUCTA, ambayo imewasilisha Kaulimbiu inayosema ***''Mishahara na Maslahi bora kwa Wafanyakazi, ndiyo kilio chetu : na Kazi iendelee''***. Kaulimbiu hii imebeba ujumbe muhimu unaolenga kuboresha maslahi ya wafanyakazi. (***Nafahamu ujumbe wa aina hii mmekuwa mkiuwasilisha mara kwa mara katika maadhimisho haya miaka kadhaa lakini leo mmeamua maneno haya ndiyo yawe Kaulimbiu na nimewaelewa vyema).***

Kwa ujumla, Kaulimbiu hii inabeba changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyakazi kama

zilivyowasilishwa na kufafanuliwa na Katibu Mkuu wa TUCTA. Kwanza, ni kuhusu viwango vya mishahara ambapo ninakubaliana nanyi kabisa kwamba viwango vya sasa havikidhi mahitaji ya mfanyakazi pamoja na familia yake, hususan nyakati kama hizi ambapo gharama za maisha zimepanda.

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Ili kuendelea kulinda maslahi ya wafanyakazi, ninatambua jukumu la Bodi za Kima cha Chini cha Mishahara katika kuishauri Serikali kuhusu upangaji wa Kima cha Chini cha Mishahara pamoja na masharti mengine ya ajira katika sehemu za kazi. Hivyo, Serikali imeshaunda Bodi za Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta zote, sekta ya Umma na sekta ya Binafsi na tayari zimeshaanza kufanya tathmini ili kufanya maboresho ya Kima cha Chini cha Mshahara kilichopo sasa. Kwenye jambo hili, naziagiza Wizara zinazohusika na

usimamizi wa Bodi hizi kuhakikisha Bodi zinawezeshwa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufasaha na kwa lengo lililokusudiwa.

*Ndugu Wafanyakazi:*

Kuhusu suala la kodi katika mishahara, itakumbukwa kwamba mwaka 2012, kiwango cha kodi kilikuwa zaidi ya **asilimia 18** lakini, baada ya majadiliano kati ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi, kiwango kikashushwa hadi tarakimu dijiti moja ya **asilimia 9** kwenye kima cha mshahara kinachozidi **shilingi 170,000**. Na kuanzia mwezi Julai mwaka jana 2021, Serikali ilivuka malengo ya makubaliano na kupunguza kodi ya PAYE hadi **asilimia 8,** na papo hapo, kuongeza kiwango cha mshahara kinachokatwa kodi kutoka **shilingi 170,000** hadi **shilingi 270,000**. Imani yetu kwamba kitendo hicho, kimepandisha kiasi fulani cha fedha katika mishahara ya wafanyakazi.

Hatua hii imewezesha kuongeza kiwango cha mshahara kama nilivyosema kinachobaki kwa mtumishi *(Net Salary)* na hivyo kuboresha maslahi yake. Pamoja na hatua hizo, Serikali imechukua hatua nyengine kadhaa za kuongeza pato la mfanyakazi kama ilivyoelezwa na walionitangulia kusema lakini hasa katibu mkuu na Rais wa TUCTA. Lakini mimi nataka niseme na niseme ni kwa kiwango gani Serikali imejitoa kupandisha kipato cha mfanyakazi.

Nilisema pale Mwanza na nakubaliana na Katibu Mkuu wa TUCTA kwamba mimi ni mama na mama ni mlezi. Na kwa maana hiyo ilinisukuma kuchukua hatua zifuatazo mwaka uliopita wa fedha :

1. Kupunguza kiwango cha PAYE ile kodi ya mshahara na kwa punguzo lile Serikali ilisamehe kukusanya kiasi cha Bilioni 14.178 ambazo zilibaki kwenu wafanyakazi.

2. Lakini tuliongeza umri wa Bima kutoka miaka 18 wa Watoto hadi miaka 21 na katika kipindi cha mwaka mmoja tumesajili watoto 65,353 ambao kama wangelipiwa matibabu yao wazazi wangetoa bilioni 3.7 kulipia matibabu yao lakini Serikali imewapokea mzigo huo na kufanya kipato kibaki kwenu.

3. Tozo ya asilimia 6 ya Elimu ya Juu pamoja na tozo ya Adhabu kuchelewa kulipa ya asilimia 10. Tozo ya asilimia 6 ambayo kwa kuisamehe mwaka mmoja serikali imepoteza bilioni 50 lakini papo hapo mnafahamu kwamba kwenye hilo suala la elimu ya juu kulikuwa kuna madeni chechefu yanayofika trilioni 1.1 nayo serikali iliamua kuyafuta. Kwenye hili Serikali hapa imesameshe Trilioni 1.168.

4. Lakini pia tulipandisha vyeo Watumishi 198,215 ambao kupanda vyeo kule kumeendana na kupanda kwa mishahara yao na Serikali ilitumia shilingi Bilioni 41.

5. Tulifanya ubadilishwaji wa Kada au Miundo wa Utumishi -Watumishi 21,204 walifaidika kwenye hilo na Serikali hapo ililipa bilioni 4.3.

6. Malimbikizo (*arrears*) ambazo tumezilipa kwa watumishi 75,007 = shilingi bilioni 124.3 zilitumika.

7. Lakini vilevile tulitoa ajira Mpya ambazo Serikali ilibidi kutumia shilingi bilioni 1.1

   Kwa hiyo ukifanya mahesabu ya fedha zote hizo, zote zilibaki kwenu wafanyakazi. Tungetangaza kiwango cha mshahara wakati ule, tukasema kima kadhaa, kisingefikia fedha hizi ambazo tumeziachia zibakie mikononi mwenu.

   Kwahiyo niliposema mimi ni mama na ni mlezi, nilikwenda kuangalia mambo haya na ninaendelea kuyaangalia katika mwaka ujao wa fedha.

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Limetajwa pia suala la malipo ya mafao na nauli kwa wastaafu. Ninashukuru kwamba mmetambua na kupongeza jitihada zilizofanywa na Serikali ambazo Mwezi Disemba

mwaka jana, Serikali ilitenga jumla ya **Shilingi Trilioni 2.17** kwa ajili ya kulipa deni la mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) **na LAPF**.

Aidha, kutokana na kuboresha huduma kwa wastaafu, ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kielektroniki ambao umeunganishwa na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), malipo ya mafao yameanza kufanyika ndani ya **siku 60** kama inavyoelekezwa na Sheria. Hii imetokana na kurahisishwa kwa uhakiki wa taarifa za wanachama, uandikishaji na uwasilishaji wa michango bila kulazimika kufika katika Ofisi za Mifuko. Na hapa natoa rai kwa TUCTA kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa taarifa na elimu kwa wafanyakazi kuhusu maboresho yaliyofanywa na Serikali au Serikali yao sikivu.

Vilevile, kwa kuwa taarifa za wafanyakazi kustaafu huwa zinajulikana na mwajiri miezi sita kabla mtumishi kustaafu, ninawaagiza waajiri waandae malipo ya Wastaafu wanaotarajia kabla ya tarehe ya kustaafu ya mtumishi au kabla Mtumishi kuondoka ofisini awe ameandaliwa stahiki zake zote na mafao yake yote.

Lakini kubwa zaidi, ni kwa waajiri kuhakikisha kwamba taarifa za watumishi wao ziko kikamilifu katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Kwasababu kuna usumbufu mkubwa, watumishi wanastaafu wasubiri mtandao uwaambie umetiliwa/hamna kitu. Wakienda ofisi za mifuko wanaambiwa taarifa hazikutimia.

Hawezi kurudi ofisini mana ameshastaafu ameondoka kwa hiyo anapata usumbufu nenda rudi, panda shuka. Sasa naagiza ndani ya kipindi cha **miezi sita (06)** ambacho mtumishi anatoa taarifa kwamba ikifika tarehe kadhaa natakiwa

kustaafu, maafisa rasilimali watu kushughulikia haki na stahiki za mfanyakazi huyu.

Halikadhalika, Mifuko nayo ifanye uhakiki wa malipo ya wastaafu ndani ya **miezi sita (06)** ili mstaafu anapomaliza anapofikiwa na tarehe ya kuondoka, malipo yake/ mafao yake yawe tayari badala ya kumzungusha nenda huku, fuatilia haki zako kule, nenda rudi zikatike, wafanyakazi wastaafu wapate haki zao haraka.

Sambamba na suala la malipo ya mafao, limetajwa pia suala la kupanga kikokotoo kitakachotoa faraja kwa wastaafu. Nashukuru Katibu Mkuu TUCTA umekwenda mpaka kutaja kiwango. Tulikuwa kwa muda mrefu tukivutana kutoka 25 kwenda 50 lakini leo TUKTA wamesema tukutane katikati.

Sasa Serikali tutakwenda kukaa katika UTATU wetu au sisi na TUCTA kuangalia tunavyoweza kufanya lakini wazo mlilokuja nalo si baya. Ombi langu kwenu TUCTA mtoe ushirikiano wa kutosha katika jambo hili ili kwa mwaka huu tuweze kulimaliza. Kikokotoo kifanikiwe na maslahi ya watumishi yaweze kupatikana na kwa kiwango kawaida maslahi huwa hayaridhishi siku zote. Mshahara huwa hautoshi siku zote. Mafao huwa hayatoshi siku zote lakini angalau yaridhishe. Mtumishi akitoka awe ameridhika na kile anachopewa. Kwa hiyo tulifanyieni kazi pamoja.

***Waheshimiwa Viongozi;***

***Ndugu Wafanyakazi:***

Natambua pia changamoto za utoaji huduma kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Na ili kutatua changamoto hizo, Serikali imeendelea kuboresha Kitita cha Mafao ya Huduma za Afya ambacho hutolewa kwa kuzingatia

Miongozo ya Tiba na Orodha ya Tiba ya Dawa Muhimu pamoja na Miongozo mingine inayotolewa na Wizara ya Afya.

Vile vile, Serikali imepokea mapendekezo ya kuongeza umri hili nimeshalisema umri wa watoto ambalo tumeshalifanyia kazi na wafanyakazi wameanza kushughulika nalo. Lakini hili la kuongeza huduma ndani ya Bima ya Afya tutakwenda kulifanyia kazi tuonea jinsi tutakavyoweza kuliamua.

Aidha, natambua pia changamoto ya wastaafu kukosa huduma kutokana na kuchangia Mfuko wa Bima ya Afya katika kipindi cha chini ya **miaka 10**. Ili kuishughulikia changamoto hii, Serikali ipo katika hatua za mwisho kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2021, ambapo, pamoja na mambo mengine, ushauri utatolewa kwa Serikali kuhusu namna bora

ya kugharamia kundi hili la wastaafu bila kuathiri ustawi na uendelevu wa Mifuko yenyewe.

*Ndugu Wafanyakazi:*

Hatua nyengine zilizochukuliwa ili kutatua changamoto ya ucheleweshaji wa makato ya wafanyakazi katika Mifuko ya Bima ya Afya ni kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai mwaka uliopita wa 2021, Serikali ilianzisha Mfumo wa kupeleka makato moja kwa moja kutoka Hazina kwenda kwenye Mifuko bila kupitia kwa waajiri. Hatua hii imepunguza malalamiko ya wafanyakazi kuhusu kutokupeleka au kutokupata huduma kwa wakati. Aidha, kwa waajiri wanaochelewesha kuwasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko, umewekwa utaratibu wa kusubiri kupata michango kutoka kwa waajiri kwa kipindi cha mwezi mmoja *(yaani grace period)* kabla ya kuchukua hatua stahiki za kuhakikisha waajiri wote wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria.

*Ndugu Wafanyakazi :*

Kumekuwa na malalamiko kuhusu vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji katika baadhi ya sehemu za kazi. Mara nyingi, vitendo hivi vimekuwa vikifanywa na baadhi ya waajiri pamoja na viongozi wa umma kinyume na Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utumishi wa umma.

Aidha, Sheria ya Tawala za Mikoa **Na. 19** ya **Mwaka 1997** imewapa Mamlaka Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kumweka Mahabusu mtumishi wa umma aliyefanya kosa ambalo linahatarisha usalama wa watu wengine au usalama wake binafsi kwa **masaa 48**. Lakini nataka niseme kwamba, nikubaliane na malalamiko ya TUCTA kifungu hiki cha Sheria kinatumika vibaya. Baadhi ya maeneo, mfanyakazi atakaposimama na kuthubutu kusema ukweli basi anakumbana na kifungu hiki cha Sheria.

Niwaombe wote waliopewa mamlaka ya kutumia kifungu hiki, wakitumie kama kifungu kilivyowekwa. Lakini kuhusu unyanyasaji sehemu za kazi, maeneo mengine, kwenye sekta binafsi lakini hata katika mashirika ya umma hilo nalo nimeagiza Wizara na Kamisheni ya Kazi wafuatilie kwa karibu sana vitendo hivi na wachukue hatua zinazostahiki.

***Ndugu Wafanyakazi Wenzangu:***

Mtakumbuka wakati wa Sherehe za Mei Mosi Mwaka jana 2021 Jijini Mwanza, nilitoa maelezo au maelekezo kuhusu Taasisi 40 ambazo zilikuwa hazijaunda Mabaraza ya Wafanyakazi kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria. Nimearifiwa kuwa, hadi kufikia Mei, 2022, jumla ya Taasisi 27 kati ya 40 zimshaeunda Mabaraza ya Wafanyakazi. Na hapa nataka nisisitize, kuunda Baraza ni jambo moja lakini kuwapa haki Mabaraza kufanya mikutano yao ni jambo la pili. Naomba nisistize sana wakuu wa sehemu za kazi waachie mabaraza

yafanye mikutano yao kwa mujibu wa Sheria, kwasabbau mabaraza ndio majukwaa ambapo wafanyakazi wanaweza kusema yale yote yanayowasibu.

Ninafahamu pia kuwa Sheria haiwalazimishi waajiri na wafanyakazi katika Sekta Binafsi kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi. Hata hivyo, naendelea kuisihi sekta binafsi kuwaruhusu wafanye mabaraza yao ya kazi kwasababu kupitia mabaraza haya ndoio watazielewa changamoto zinazowasibu wafanyakazi wao na kuweza kuzichukulia hatua Na kuepukana na kadhia ya kuja kupambana na Kamisheni ya Kazi au Wizara inayoshughulikia mambo ya kazi.

***Ndugu Wafanyakazi;***

Naomba sasa mniruhusu nizungumzie kidogo suala la watumishi wa umma wa darasa la saba au wale

walioondoshwa kwa vyeti feki . Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilichukua hatua kadhaa katika nyakati mbalimbali kuwarudisha watumishi wad arasa la saba wale ambao labda waliondoshwa kwa makosa lakini wale ambao baada ya kutoka wameenda kujiendeleza na wamepata sifa zinazotakiwa wamerudishwa makazini kwa mamia.

Lakini nimepokea malalamiko ya TUCTA kuhusu darasa la saba ambao wameondoshwa pamoja na mkumbo ule wa vyeti feki. Baada ya kikao changu na TUCTA na Mawaziri wanaohusika tulikaa tena kikao cha Serikali peke yetu na tumeweza kuja na mambo yafuatayo :-

Wale wote waliofukuzwa, walifanya kazi kwa muda mrefu lakini wakafukuzwa kwa ajili ya vyeti feki na kwamba hawakupata chochote cha kuondoka nacho, nimewaagiza Wizara pamoja na Wizara ya Fedha waangalie ni kiasi gani wafanyakazi wale walikatwa kwenye jasho la mishahara yao,

kile walichochangia kwenye mifuko, kwenye jasho la mishahara yao waweze kulipwa. Kile walichokatwa nadani ya mishahara yao asilimia 5, tuache asilimia 10 ya mwajiri. Lakini vilevile niliwaambia waangalie watumishi wote waliofanya kazi kwa muda mrefu na wakabakisha mwaka 1/ 2 kustaafu na wenyewe wawaangalie ni kiasi gani kitatugharimu, kama tutawapa mafao yao baada ya utumishi wao wa muda mrefu.

***Ndugu Zangu Wafanyakazi Wenzangu:***

Lipo pia suala la makato ya mikopo ya Elimu ya Juu ambalo kama nilivyoelekeza mwaka jana kwenye Sherehe ile **asilimia sita (06)** tumeitoa. Lakini kulikuwa na jengine kwamba waliokopa walikopa kwa sheria mbili tofauti moja inakata asilimia 8 na nyingine inakata asilimia 15 na wakaomba kuwa wale wa asilimia nane waendelee na makataba wao lakini hili Serikali nataka niwaambie hapa tumelikataa. Wote watakwatwa kwa asilimia 15.

*Ndugu Zangu Wafanyakazi Wenzangu:*

Naomba sasa mniruhusu nijielekeze kwenye masuala mbalimbali yahusuyo hali ya ajira nchini. Kwanza, kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa ajira za wageni nchini, Serikali ilitunga Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni **Na. 1 ya Mwaka 2015.** Kwa mujibu wa Sheria hii, Vibali vya Kazi kwa wageni hutolewa kwa kuzingatia sifa za kielimu, ujuzi na uzoefu wa kazi. Aidha, Sheria hii inawataka waajiri kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kurithisha Ujuzi kwa Wazawa. Vilevile, ili kulinda ajira kwa wazawa, Sheria husika inawataka waajiri kuwa na uwiano wa **1 : 10** kwa wafanyakazi wageni na wazawa. Nataka niwahakikishie kuwa, pamoja na kuvutia uwekezaji na uhawilishaji maarifa na ujuzi kutoka nje ya nchi, Serikali itaendelea kuhakikisha wageni wanaopata vibali vya kazi ni wale tu wanaostahili kwa mujibu wa Sheria.

Katika kikao changu na TUCTA juzi waliniambia baso kuna wafanyakazi ambao kisheria hawastahiki kuwepo lakini bado

wapo nchini na nimeitaka Wizara na Kamisheni ya Kazi walifanyie kazi kwa haraka na waje kuniambia hali halisi ilivyo.

Imetajwa pia changamoto ya Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira kukiuka Sheria za Kazi. Serikali inatambua uwepo wa changamoto hii ambapo imeshaanza kuzifanyia marekebisho Sheria na Kanuni ambazo zinasimamia uendeshaji wa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira ili kuhakikisha wanabaki na jukumu lao la msingi ambalo ni kuunganisha watafutaji kazi na waajiri badala ya wao kuwa sehemu ya waajiri, jambo ambalo linaathiri sana maslahi ya wafanyakazi katika Sekta Binafsi. Hili halikubadili kwa vigezo vyovyote.

***Ndugu Wafanyakazi:***

Serikali inatambua tatizo la kukinzana kwa Sheria za Kazi ambako kunasababisha migongano hasa kwenye Sekta ya Utalii inayowahusu lile kundi wanaloliita Jeshi Usu. Kuhusu hili

niliwataka TUCTA na Serikali wakae waangalie Sheria zinavyosema na wakubaliane ipasavyo

Aidha, kuhusu ufungaji wa Mikataba ya Hali Bora, Motisha za wafanyakazi na masuala mengine, hakuna budi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotumika katika Utumishi wa Umma. Taasisi za Umma zinapaswa kuwasilisha Mikataba hiyo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinishwa kwa mujibu wa Sheria.

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Nafahamu kuwa marekebisho ya Miundo ya Kiutumishi (Schemes of Service) yaliyofanywa na Serikali yameongeza muda wa mtumishi kukaa kwenye cheo kimoja kabla ya kupanda sambamba na kuongezeka kwa vyeo chini ya kada husika. Niwahakikishie kuwa marekebisho haya ni ya msingi

kwani yataondoa tatizo la watumishi kupanda vyeo bila kuwa na uzoefu wa kutosha pamoja na kuimarisha dhana ya ukuu kazini *(Seniority)* ili kuhakikisha wafanyakazi wanaiva kabla ya kupandishwa vyeo.

***Ndugu Wafanyakazi:***

Tangu tupate uhuru, nchi yetu imeridhia jumla ya **Mikataba ya Kimataifa ipatayo 38**. Hata hivyo, kati ya mwaka **2017 hadi 2019**, Serikali ilijiondoa katika Mikataba **mitano (05)** ambayo haikuwa inaendana na hali yetu Tanzania baada ya kuona kwamba haina tija. Hivyo, imebaki **Mikataba 33** ambapo Mikataba **nane (08)** ni ya msingi na maalum kwa Nchi wanachama kuipa kipaumbele katika utekelezaji wake *(Core Conventions)* kwa kuwa inagusa Haki za Binadamu za msingi.

Hata hivyo, Mkataba **Na. 189** unaohusu Wafanyakazi wa Majumbani, Mkataba **Na. 190** unaohusu Ukatili na Unyanyasaji

pamoja na Mkataba **Na. 155** unaohusu Usalama na Afya sehemu za kazi ipo katika ngazi mbalimbali za maamuzi kwa lengo la kuona uwezekano wa kuiridhia. Na hapa ninapenda niwakumbushe kuwa katika kuridhia Mikataba ya Kimataifa, lazima tuzingatie vigezo kadhaa, ikiwemo umuhimu wa Mkataba kwa nchi yetu, lakini mila na desturi zetu pamoja na utayari katika utekelezaji wa Mikataba husika. Kwa mfano katika Mkataba wa haki za wafanyakazi majumbani, kuna kipengele kinasema mfanyakazi wa nyumbani apewe haki zote pamoja na haki za faragha ; mkataba unasema mfanyakazi wako wa nyumbani umtengee chumba na kama ana mwenziwe basi wahamie hapo. Kwa kila na desturi zetu na tulivyozoea Watanzania kifungu hiki hakitekelezeki. Sasa kuna vifungu vya aina hivyo ndani ya hiyo mikataba, tunayopigiwa kelele Tanzania hatujairidhia. Kwahiyo tunaendelea kupitia vifungu kwa vifungu tuone vile ambavyo havitufai na tuandike mikataba ilikotoka tuombe kwamba mikataba hii

kwenye vifungu hivi tanzania tunaona haviko sawa na sisi. Kwahiyo hatukatai mikataba ya kimataifa hasa hii ya Shirika la Kazi Duniani lakini iendane na Mila na desturi na hali yetu ya Tanzania.

***Ndugu Wafanyakazi wenzangu:***

Wakati nikielekea kuhitimisha, napenda nisisitize kuhusu masuala kadhaa ya jumla:

- Kwanza, limejitokeza tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa kiholela, kinyume na uhalisia wa mazingira yetu na kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu nafahamu umeshalitolea maelekezo na mimi nasisitiza : Wafanyabiashara tuache visingizio, twende kwenye uhalisia;

- Pili, lipo suala la ndugu zetu wamachinga na bodaboda ambalo nilishalitolea maelekezo kwamba wawekewe utaratibu na siyo kuwazuia kufanya shughuli zao. Wawekewe utaratibu waweze kufanya shughuli zao za kujiingizia kipato. Nimeshaletewa malalamiko kutoka baadhi ya maeneo na ninayafanyia kazi. Nataka viongozi mtumie busara zaidi na siyo mabavu katika kushughulikia kero za wananchi. Lakini shughuli hizi zinapendeza zikifanyika mchana kuliko kuvizia usiku na kwenda kuvuruga na kwenda kuwaondoa mahali walipo.

  Kwahiyo niombe sana viongozi hasa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kufuata maelekezo niliyoyatoa.

- Tatu, kumeanza kujitokeza vitendo vya kihalifu vinavyotishia usalama wa wananchi pamoja na mali zao.

Kuna vijana wanajiita « panya road » ***(au panya buku)*** wanavamia, kujeruhi na kupora. ***Nawaonya waache mara moja unyama huo na kama wanahatarisha maisha ya wananchi, usalama na mali za raia basi wajue maisha yao pia yamo hatarini***. Kwa hiyo nawaonya waache mara moja.

Na kabla ya kuhitimisha, yapo malalamiko kutoka **Vyama 19** vya Wafanyakazi wa Sekta Binafsi vinavyodai kutengwa na TUCTA na kwamba havishirikishwi kikamilifu katika Sherehe za Mei Mosi. Naiagiza Wizara na TUCTA kuona namna bora ya kuwashirikisha katika umoja huo wa wafanyakazi wa Watanzania.

Mwisho, niwakumbushe na nafurahi kwamba vikundi kadhaa vilivyopita pale wamekumbusha kwamba **tarehe 23**

**Agosti, 2022** kutakuwa na zoezi la kuhesabiana, zoezi la Sensa. Niwakumbushe kila mmoja wetu ajitokeze.

Mwisho kabisa ; **niseme nisiseme!** Ulezi wa mama unaendelea yale tuliyoyafanya mwaka huu, mambo mbalimbali, kupunguza kodi kuona hiki kuona hiki tutaendelea kuyafanya. Lakini pamoja na hayo, lile jambo letu lipo.

Ndugu zangu, jambo letu si kwa kiwango kilichosemwa na TUCTA kwasababu mnajua hali ya uchumi ya nchi yetu na hali ya uchumi wa dunia. Hali si nzuri sana. Uchumi wetu ulishuka chini mno. Tumejitahidi sana. Na kwasababu tulishatoa ahadi mwaka jana, kwahiyo nimeagiza jambo liwepo, mahesabu yanaendelea tuatajua lipo kwa kiasi gani. Lakini jambo lipo.

Baada ya kusema hayo, lakini ndugu zangu niseme jambo moja, wakati mnapita na mabango hapa ya maandamano, nilikuwa naangalia bango linalosema tutafanya kazi kufa kupona uchumi ukue, sijaona. Sijaona hata moja. Lakini Katibu Mkuu wa TUCTA wakatia anatetea viwango vya mishahara anasema tulifanya utafiti mara mbili, viwango vya chini ni hivi. Lakini hakufanya utafiti wa tija inayochangiwa na wafanyakazi ndani ya uchumi.

Kwasababu hiyo ndiyo ingekuwa msingi wa majadiliano bain aya Serikali na vyama vya wafanyakazi. Kwamba kwa mwaka huu wafanyakazi wamechangia tija kiasi hiki, kwa hiyo huo ndio msingi wa majidliano. Utafiti huo hawajafanya. Lakini wakati ukifika wanadai tu, wanadai, wanadai. Naomba fanyeni utafiti wa aina hiyo pia. Lakini hayo ninayoyasema hayaondoi jambo letu, jambo letu lipo.

Baada ya kusema hayo, niwatakie utekelezaji mwema wa majukumu yenu katika sehemu zenu za kazi na Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**Solidarity --------------- ?**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!**